Bustani Yako Inakuwaje?

Na

J. D. Logan

(How Does Your Garden Grow?)

Bustani Yako Inakuwaje?

Na

J. D. Logan

Novemba 5, 2011

Bustani Yako Inakuwaje?

Swali hilo hapo juu uulizwa katika nyimbo za shule ya awali, “Mariam, Mariam, ni kunyume sana”. Tunapoandaa sehem ya udongo wetu wenye changarawe wa Magharibi mwa Washington kwa ajili ya kupanda mbegu, imetokea kwangu kwamba somo hili linaweza kuwafaidisha wote. Ni majibu yaapi tunayoweza kupata katika neno la Mungu?

Udongo Ni Lazima Uandaliwe

Kuna kila aina ya udongo duniani. Yote inapaswa kuandaliwa kwa ajili ya kupanda. La sivyo, mtu hawezi kutarajia mavuno.

Hosea aliwaambia Waisraeli (ambao walitenda dhambi mbaya zaidi) katika Hosea 10:12, “*Jipandieni katika haki, vuneni kwa fadhili; uchimbueni udongo wa mashamba yenu, kwa maana wakati umewadia wa kumtafuta BWANA, hata atakapokuja na kuwanyeshea haki.*” “Uchimbueni udongo” ni ardhi isiyo na rutuba. Israeli hawakuwa na rutuba kwa sababu ya dhambi zao zao. Na ndivyo ilivyo kwetu. Kama tukiwa na udhaifu (dhambi) hatuwezi kuzaa “matunda ya Roho” (Gal. 5:9).

“Kuchimba” inamanisha kutifua. Utifuaji ndio mfumo unaokubalika katika maandalizi ya udongo. Kristo alisema sote “*tushike jembe na kulima*”, lakini sio “*kuangalia nyuma*”, la sivyo hatufai katika ufalme wwa Mungu. (Luka 9:62).

Tunapolima, tunapaswa kufanya hivyo tukiwa na matumaini. “*Au yamkini anena hayo kwa ajili yetu? Naam, yaliandikwa kwa ajili yetu; kwa kuwa alimaye nafaka ni haki yake kulima kwaa matumaini, naye apuraye nafaka ni haki yake kutumaini kupata sehemu yake.*” (1 Kor. 9:10). Tumaini letu ni kupata mavuno mengi. “*Nyingine zikaanguka penye udongo mzuri; zikamea, zikazaa moja kwa mia. Alipokuwa akinena hayo alipaza sauti akisema, mwenye masikio ya kusikiliza, na asikie.*” (Luka 8:8). Mamia yanaweza kuchukulia kama mavuno mazuri!

Hivyo basi, maandalizi ya udongo ni muhimu zaidi kwa ajili ya mavuno mazuri. Lakini vipi kama tusipoandaa udongo tunavyostahili?

Njia Mbaya

Mtu anawezaa kukataa udongo wake kwa njia nyingi. Matokeo yaanawezaa kubashiriwa. “*Mtu mvivu hataki kulima wakati wa baridi; hivyo wakati wa mavuno ataomba, hana kitu.*” (Mit. 20:4) Matokeo ya kubashiri!

Yesu alitufundisha mengi kuhusu maandaalizi ya udongo. “*Mpanzi alitoka kwenda kwenda kupanda mbegu, na alipokuwa akipandaa, zingine zilianguka njiani; zikakanyagwa, ndege wa angani wakaja wakala.*” (Luka 8:5).

“Njiani” siyo ardhi ya kulima. Ni nani awezaye kupanda mbegu pembezoni mwa njia? Haishangazi kwamba baadhi ya mbegu “zilikanyagwa” na zilizobaki zikaliwa na ndege. Matokeo yanayotarajiwa: hakuna mazao!

“*...zingine zilianguka mwambani…*” (Ms.6). Sisi, tulio Magharibi mwa Washington, tunafahamu ardhi yenye changarawe. Mtu hapandi mbegu kwenye changarawe alafu atarajie mavuno. Hivyo ikipandwa, mazao yatanyauka, hazitastawi. Udongo usiotifuliwa hauwezi kutoa mavuno!

“*...zingine zilianguka kati ya miiba, na miiba ikamea pamoja nazo ikazisonga.*” (Ms.8). udongo usioandaliwa utakuwa na magugu, mbegu isiyo bora, mizizi, n.k. Hizi zipo katika ulinganifu wa moja kwa moja na mbegu iliyopandwa na itakuwa katika ustawi muhimu wa mavuno mengi. Mazao yatasongwa!

Njia Mbaya Ya Kulima

Wengine hulima, hata kama inapendekezwa sana, lakini haifanyiki vizuri. Matoke hutabirika.

Sulemani anatufundisha, “*...hata ukulima wa waovu, ni dhambi.*” (Mit. 21:4) tunapojiingiza kwenye dhambi matokea ni hitimisho ya muda mrefu. “*Msahara wa dhambi ni mauti.*” (Rum. 6:23).

Hosea ananena kuhusu Israeli, “*Mmelima dhuluma, mmevuna uovu; mmekula matunda ya uongo; kwa maana uliitumainia njia yako, na wingi wa mashujaa wako.*” (Hos. 10:13). Matokea yanaeleweka; lima uovu ili uvune dhambi. Hakuna mavuno ya mazao!

Wakati Wa Kupanda

Udongo ukiwa umeshaandaliwa, wakati wa upandaji unafuata. Maandalizi ya udongo ukishafanyika, ni muhimu kuweka mbegu ardhini. Kuna njia mbili ambazo tunaweza kupanda isivyo.

Usipande kitu

Kutofanya chochote baada ya kuandaa udongo kikamilifu ni ujinga mgumu. Matokeo yanaweza kuwa katika hali mbaya kuliko ya mwanzo.

Yesu anatufundisha, “*Pepo mchafu amtokapo mtu hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzika, asipoona husema, nitairudia nyumba yangu niliyotoka. Hata afikapo, akaiona imefagiwa na kupambwa ndipo huenda akachukua pepo wengine saba, walio waovu kuliko yeye mwenyewe, wakaingia na kukaa humo; na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza.*” (Luka 11:24-26).

Tatizo la kawaida hapa ni kwamba mtu anayesemwa alisafisha “roho wachafu”, hakuweka chochote katika sehemu yake. Kwa vile hakuna chochote ambacho kinaweza kukaa katika chupa, matokeo ni hitimisho yaliyokwenda sana. Mbadala “udongo” kwa “mwanaadamu” na “mbegu”

kwa “roho” na tunaona wazi kwamba tunaposafisha, lima na uandae udongo kwa ajili ya kupanda, ni lazima tupande mara moja. La sivyo, mbegu zitasongwa, na kutunyima mavuno mazuri.

Panda Mbegu Mbaya

Paulo anatufundisha kwamba “*...yeye apandaye katika mwili huyo katika mwili atavuna uharibifu;...*” (Gal. 6:8). Mpumbavu ni mtu yule atakayepanda mbegu na mbigili katika udongo uliolimwa vibaya. Kwa hitimisho gani? Matokeo yanajulikanaa: “*...apandacho mtu ndicho atakachovuna.*” (Gal. 6:7).

Tunapaswa kukataa mbegu mbaya ambazo huathiri mbegu njema. Biblia inatuambia kuhussu “magugu”. Gugu ni mmea ambao haufaaia kwa mwanadamu (wengine husema kuwa hulewesha) lakini hufanana na ngano. Kama mtu aakidanganywa akapanda gugu badala ya ngano, atakuwa mbavu kweli. Ni aina gani ya zao ambalo atatarajia kuvuna? (angalia Mat. 13:37-42).

Wazo lingine kuhusu upandaji usio mzuri. Tunapaswa kupanda mbegu nyingi ili kuenea ardhi vizuri. Kama mbegu ikipandwa vibaya, kuna sehemu zingine za uwazi na, kama matokeo na ubaya, palizi, magugu, mbigili, n.k hukua, huaribu mazao (angalia 2 Kor. 9:6).

Panda Vizuri

Baada ya kuandaa ardhi vizuri na kutofanya kosa katika kulima, mbegu mbaya, hakuna mbegu, nk., lazima tupande mbegu zetu vizuri tukitarajia mavuno mazuri.

Yesu anatufundisha kwamba “*Mbegu ni neno la Mungu.*” (Luka 8:11). Anaendelea kufundisha, “*Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tenaa ni uzima.*”

Kama tukipanda neno la roho, tuta “*...vuna uzima wa milele.*” (Gal. 6:8).

Mbegu hii inaweza ikawa ndogo, lakini ikabeba sehemu kubwa ya muhimu katika mavuno. Yesu anatufundisha kuwa na imani “*mkiwa na imani kiasi cha punje ya aradali.*” (Mat. 17:20) na kwamba mbegu hii “*ingawa ni ndogo kuliko mbegu zote zilizo katika nchi.*” (Marko 4:31) inaweza, na mara zote inaweza, kukua katika sehemu kubwa.

Lazima tupande mbegu hii kwa wingi. Paulo anatufundisha kwamba “*Lakini nasema neno hili apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu.*” (2 Kor. 9:6).

Kuyajali Mazao

Ni muhimu kuhudumiaa mazao yetu kwa bidii. Mkulima mwerevu atatumia muda wake mwingi katika shamba lake akiangalia mazao yake. Mara nyingi, lazima achimbe uoto mbaya, amwagilie, mvua zinapopungua, na kwa njia zozote aangalie hali ya mazao yake.

Haipendezi kupanda mbegu mbaya. Uvivu (kutofanya kazi, uvivu) utaruhusu kusongwa na hivyo kuharibu mbegu njema. Mazao mazuri yanahitaji umakini!

Paulo anatufundisha somo hili wazi. "*Tusichoke kutenda mema, maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho.*" (Gal. 6:9).

Neno "zimia" hutokana na neno la Kiyunani "eklue" ikimanisha "pumzika". Hivyo tunaona kwamba tukishalima, kuandaa, na kupanda katika udongo wetu, hatupaswi kupumzika na kuacha mazao yetu, maana kuna hatari nyingi ambazo zinaweza kuzuia mavuno yetu kama tukiacha kwa uvivu!

Ndugu, bustani yetu inakuwaje?

Ikiandikwa katika upendo wa kweli,

J D Logan.